# MAMBO AMBAYO WANAWAKE WAZEE WAWAFUNDISHE WANAWAKE VIJANA

DR STANSLAUS GEORGE MWANISAWA

# TARATIBU ZA KISHERIA

***Mambo ambayo wanawake wazee wawafundishe wanawake vijana*** @2021

Kitabu hiki kimeandikwa na Stanslaus George Mwanisawa. Ni marufuku kusambaza, kunakili au kutumia sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi. Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa haki za mwandishi unaoweza kupelekea mashitaka toka kwa waandaaji wa kazi hii.

Haki zote zipo chini ya Stanslaus George Mwanisawa.

@Haki zote zimehifadhiwa.

ISBN 978 -9912 9851-1-7

**Mawasiliano**;

**Simu**; +255 755668825/ 0622552227
**Baruapepe**:Stanslausmwanisawa23@gmail.com
**Facebook / instagram:** you are worthy ministry
Dar es salaam, Tanzania

## SHUKRANI

Ninamshukuru Mungu kwa kunipa neema, maarifa na hekima ya kuandika kitabu hiki, haikuwa kazi rahisi lakini kila wakati nalijitia nguvu katika Bwana mpaka kukamilika kwa kitabu hiki.

Ninamshukuru mama yangu Albertina F. Kalimalwendo na familia yangu kwa ujumla kwa maombi yao na kwa kunitia moyo. Mungu awabariki sana.

Shukrani zangu za dhati ziende kwa kila aliyehusika katika kuhakikisha kitabu hiki kinakamilika kwa wakati.

Mwisho, ninawashukuru sana wasomaji wangu ambao mmekuwa mkifuatilia masomo yangu na kusoma vitabu ambavyo Mungu amenipa neema ya kuandika.

Kitabu hiki kimesheheni maarifa yatakayowasaidia wanawake wazee na vijana kuwa bora, kutambua na kusimama katika nafasi zao katika familia zao.

## UTANGULIZI

Nimepata neema ya kukutana na wanawake vijana wengi, wengine wakiwa marafiki zangu wa karibu sana. Nimepata nafasi ya kujua maisha yao binafsi na kuzungumza nao juu ya mambo mengi.

Nilichogundua ni kwamba kuna kundi kubwa la wanawake vijana ambao wamefikia umri wa kuolewa, wana kiu ya kuolewa na wengine tayari wameolewa lakini hawajui vitu vya msingi kabisa vitakavyofanya ndoa zao zifanikiwe.

Wako vizuri sana kwenye eneo la kitaaluma na wengine wanafanya mambo makubwa lakini wanashida kubwa kwa sababu uwezekano wa ndoa zao kudumu ni mdogo sana na hata kama zitadumu kuna uwezekano kutakuwa na ugomvi usioisha.

Hii ni kwa sababu wengi wao kwanza, hawana mambo ambayo ni ya msingi katika maisha yao hasa ya ndoa,jambo la pili; hawajui kuwa hawana mambo hayo ya msingi na wengi

wanaamini hawahitaji kujifunza mambo hayo ya msingi katika maisha yao binafsi na ndoa zao.

Wengi hawajui vitu vya msingi katika maisha, yaani hata kazi zile za nyumbani kama kupika, kufua, usafi na kupanga vitu katika nyumba.

Shida haijaanza na wao, shida imeanza na malezi waliyoyapata tangu wakiwa wadogo na namna ambavyo wameona wanawake wazee hasa wale wa karibu wanaenenda katika familia zao.

Wanawake wazee wengi katika kizazi hiki hawana na hawajui vitu hivi vya msingi, hii imepelekea wawalee vibaya wanawake vijana.

*"Mlee mtoto katika njia impasayo naye hataiacha hata atakapokuwa mzee"*

***MITHALI 22:6***

Wanawake vijana wengi wamezishika njia mbaya ambazo wamefundishwa tangu wakiwa wadogo, na sasa hata katika ujana wao hawajazisahau na hawataki kuziacha.

Kama wangefundishwa mambo haya ya msingi tangu wakiwa wadogo basi wasingehangaika

sana ukubwani. Wako waliojawa na hofu ya kuolewa kwa sababu hawajui mambo haya ya msingi na wanajiuliza wataishije katika ndoa zao ingawa kwenye maeneo mengine kama vile taaluma wako vizuri sana.

Kuna namna ambavyo wanawake wazee hawajawa waaminifu kujifunza na kuwafundisha wanawake vijana mambo haya ya msingi. Wako wachache waaminifu ambao wamewalea watoto wao (wanawake vijana) vizuri.

Wanawake wazee wengi wanawafundisha wafanya kazi wa ndani kuwa wanawake bora wakati watoto wao wenyewe wanawalea vibaya.

Kinachonishangaza, kuna wanawake wazee ambao wao walifundishwa mambo haya ya msingi na yakawafanya kuwa wanawake bora katika familia zao lakini wao hawataki kuwafundisha wanawake vijana, wanadhani kwamba kufanya hivyo ni ushamba na kuwatesa.

Kuna kitu kilifanyika katika familia ya Timotheo ambacho naamini ni mfano mzuri wa kuigwa

*“Nikiikumbuka Imani uliyonayo isiyo na unafiki, ambayo ilikaa kwanza katika bibi yako Loisi na katika mama yako Eunike, nami nasadiki nawe unayo”*

***2 TIMOTHEO 1:5***

Ukisoma kwa umakini mkubwa utaona, bibi yake Timotheo alimwamini Yesu na kuokoka. Bibi huyu alikuwa na imani isiyo na unafiki kabisa, akamfundisha na mwanae yaani Eunike naye akamwamini Yesu na akaokoka. Eunike naye akamfundisha Timotheo imani ileile aliyofundishwa.

Sasa angalia, bibi yake Timotheo alikuwa na imani isiyo na unafiki, akamfundisha Eunike naye imani ya namna hiyohiyo na mwisho Timotheo naye akafundishwa imani ileile isiyo na unafiki.

Kwa hiyo malezi ambayo bibi yako alipata yawe ni mazuri au mabaya uwe na uhakika aliyapitisha kwa mama yako na mama yako atayapitisha kwako.

Kama ni mazuri ni heri lakini kama ni mabaya basi uwe na uhakika maisha yako yatavurugika kama usipochukua hatua madhubuti.

Kama wazazi au walezi (wanawake wazee) wamejifunza mambo ya msingi kama vile kazi za nyumbani, mwenendo safi nk watakuwa na ujasiri wa kuyafundisha mambo hayo kwa watoto wao (wanawake vijana).

Tabia na imani walizonazo wanawake wazee ndizo wanazopitisha kwa wanawake vijana. Kama wanawake wazee ni wasumbufu na wasiotulia katika familia zao uwe na uhakika na wanawake vijana watakuwa hivyo kama wasipoamka na kubadili mwelekeo.

Mwezi wa tano mwaka 2021, nilisoma habari moja iliyoandikwa na shirika la utangazaji BBC, iliyokuwa na kichwa cha habari "*kizazi cha ukahaba*". Katika habari hii uliandikwa ushuhuda wa mama mmoja ambaye alitokea katika kizazi cha kikahaba.

Bibi yake na mama huyu alikuwa kahaba, hivyo bibi akamfundisha mwanae (mama wa huyu

aliyetoa ushuhuda) tabia ileile naye akawa kahaba, yeye naye (mama aliyetoa ushuhuda) akufundishwa na mama yake tabia ileile kutoka kwa bibi akawa kahaba, bahati nzuri baada ya kupitia misukusuko katika kazi yake ya ukahaba macho yake yakafunguka, akagundua kwamba ukahaba ni kitu kibaya ambacho kimeharibu sana maisha yake.

Alipogundua hili akaamua kukata mnyororo wa ukahaba kwa kuhakikisha mtoto wake hajiingizi kwenye ukahaba. Mama huyu alihakikisha binti yake anaenda shule na kulingana na chombo hicho cha habari mama huyo alifanikiwa kuwa wa kwanza kumsomesha mtoto wake mpaka chuo kikuu katika kizazi hicho kilichoitwa kizazi cha makahaba.

Hapa nataka kukuonyesha tu namna ambavyo malezi aliyopewa mzazi wako (mwanamke mzee) yanavyoweza kupitishwa kwako (mwanamke kijana) na kuathiri vizazi kadhaa mbele.

Ndio maana ni muhimu sana kwa wazazi hasa wale wakike maana ndio walengwa wa kitabu

hiki, kuhakikisha wanapitisha malezi bora kwa wanawake vijana kwa kuwafundishwa mambo haya ya msingi yatakavyowafanya wawe bora kwenye maisha yao binafsi na kwenye familia watazobarikiwa na Mungu.

Mungu amenipa neema ya kuandika kitabu hiki ili kuwakumbusha wanawake wazee kuwafundisha vema wanawake vijana mambo ya msingi yatakayowajenga na kuwafanya kuwa wake na mama bora katika familia zao.

Lakini pia kuwakumbusha wanawake vijana kufanya jitihada binafsi za kutafuta wanawake wazee wenye sifa njema watakaowafundisha kuwa wake na mama bora katika familia zao.

## SURA YA KWANZA

## MPE MALEZI ANAYOSTAHILI

*"Mlee mtoto katika njia impasayo…"*

***MITHALI 22:6***

Wakati nasoma habari ya Samson katika kile kitabu cha waamuzi sura ya 13, nilikutana na kitu muhimu sana ambacho kilileta kiu kubwa ndani yangu kutafakari juu ya malezi katika kizazi hiki tulichonacho.

Baada ya malaika kumtokea mama yake Samson na kumpa maelekezo juu ya mimba atakayobeba, kumzaa na kumlea mtoto ambaye atakuwa na kazi maalumu ya kuwakomboa wana wa Israel kutoka katika mikono ya wamidiani.

Mama yake Samson alimshirikisha mume wake juu ya kile malaika alisema. Kitu cha ajabu sana ni kwamba mzee Manoa hakuridhika tu na taarifa alizopokea kutoka kwa mke wake, badala yake akawa na kiu ya kupata taarifa ile muhimu moja kwa moja kutoka kwa malaika.

Hivyo akamuomba Mungu yule malaika arudi tena kuwapatia maelekezo yale, baada ya muda

Mungu akamtuma malaika wake tena kwenda kuwapa maelekezo.

Nilipokuwa nikifuatilia maungumzo kati ya mzee Manoa na yule malaika kuna kitu kilinigusa sana.

Kilichonifurahisha sana ni pale nilipoona kitu mzee Manoa alitaka kujua juu ya mtoto atakayezaliwa. Ni kiu yangu kuona kila mzazi katika kizazi hiki analichukulia suala hili kwa uzito wake

"*Ndipo huyo Manoa akamwomba Bwana, akisema, Ee Bwana nakuomba yule mtu wa Mungu uliyemtuma na aje kwetu mara ya pili, ATUFUNDISHE YATUPASAYO KUMFANYIA HUYO MTOTO ATAKAYEZALIWA*"

***WAAMUZI 13:6***

Mzee Manoa alitaka kujua *"namna ya kumfanyia (kumlea) mtoto atakayezaliwa"* ili Samson aweze kutimiza kusudi la kuzaliwa kwake.

Samson alizaliwa mnazayo, yaani mtu aliyetengwa kwa ajili ya kazi maalumu, kwa hiyo kulikuwa kuna namna maalumu ya kumlea.

Kuna vitu watu wengine walikuwa wanaweza kutumia na kuvifanya lakini Samson hakuruhusiwa. Kwa hiyo kuwa na maelekezo maalumu juu ya namna ya kumlea mtoto huyu ilikuwa ni muhimu sana.

Baada ya kusoma habari hii swali lilikuja ndani yangu, *hivi ni mara ngapi wazazi wameenda mbele za Mungu kumuomba awape maelekezo juu ya malezi ya watoto?* kwa sababu kila mtoto ana kusudi lake na kuna namna anatakiwa kulelewa (kuna malezi anayostahili).

Mwanzo mzee Manoa hakujua Samson anazaliwa kwa ajili ya kazi gani na hivyo ilimbidi amuulize malaika

*“Je? Huyo mtoto atakuwa wa namna gani na kazi yake itakuwa ni nini*?”

**WAAMUZI 13:12b`**

Kwa nini mzee Manoa aliuliza juu ya kazi ya mtoto na namna atakavyokuwa? Ni kwa sababu kuna malezi maalumu Samson alitakiwa kupata ili kumuandaa kuwa yule aliyetakiwa kuwa na kutimiza kusudi lake.